Viini Vya Ukimwi na PEV (matibabu baada ya kujihatarisha)

Ukimwi (upungufu wa kinga mwilini) ni janga kuu. ugonjwa huu umepunguza kiwango cha maisha na umri wa maisha kwa watu wa nchi zinazoendelea na kuongeza gharama za nchi zilizoendelea. HIV ni virusi vinavyosababisha ukimwi. Vinaeza kuenezwa kupitia damu, shahawa, maji ya uke, majimaji ya uume, na maziwa ya mama. Kuambukiza na HIV husababishwa na uhusiano wa ngono bila mpira (kondomu) na kuchangia sindano za kujidunga madawa. Njia nyingine muhimu ya kueenea kwa HIV na kuambukizwa ni kupitia mama mja mzito hadi kwa mtoto, ambayo hutendeka wakati wa kuzaliawa na kulisha mtoto kwa maziwa ya mama.

Virusi hivi huadhiri viini vya mfumo wa kinga za mwili vinavyostahili kulinda mwili kutokana na magonjwa. Lakini HIV hutoroka na kuharibu viini hivi moja kwa moja au kwa kutumia njia nyingine. Kinga za mwili nazo hupungua na kuisha nguvu.

Ukimwi ni hali ya binadamu ambapo virusi vya HIV hufanya kinga za mwili kuishiwa na uwezo. Uharibifu wa kinga za mwili husababisha mwili kuambukizwa na magonja mengine. Hata homa huweza kusababisha kifo. Siku hizi, madaktari huuita ukimwi “hatua ya mwisho” ama HIV “iliyosambaratika”.

Kuna dalili kadhaa za kuambikizwa na HIV. Dalili hizi ni sawa na zile za homa. Dalili za kawaida ni homa, maumivu ya kijumla, uchovu, kuumwa na kichwa, jasho, maumivu ya misuli na miguu, kugonjeka na kupoteza uzito. Katika hatua ya mwisho ya ukimwi dalili hizi hazitoweki kwa sababu zimesababishwa na maambukizo yanayotokea kinga za mwili zinapopunguzwa na ukimwi.

Aidha watu wanaougua wako na uwezo mkubwa wa kupata maradhi yasiotisha mwili ulio na kinga za mwili sabamba. Maradhi haya hujulikana kama maradhi fafanuzi ya ukimwi. Kwa mfano, PCP, ugonjwa wa mapafu usiopatikana kwa urahisi kwa watu wenye afya nzuri lakini umeenea katika wanaougua kutokana na ukimwi. Katika maeneo kusini mwa Afrika, PCP ni kati ya dalili za kwanza za ukimwi kwa watu ambao hawajapimwa. Kuna maradhi fafanuzi mengine ya ukimwi. Kwa mfano, wanaouguza hupata maradhi ya mfumo wa neva kwa wingi na huwa na uwezo mkubwa wa kupata aina nyingine za kansa ambazo husababisha kifo.

Hadi sasa ukimwi hauna tiba. Madawa yenye gharamu kubwa yanaweza kupunguza kueenea kwa virusi vya HIV lakini mwishoe kila mtu anayeuguza kutokana na virusi vya ukimwi hufa mapema ikilinganishwa na mtu mwenye afya nzuri.

Ili usiambukizwe na HIV lazima utilie maanani kutumia mpira kila wakati. Hata watu walio na mpenzi wa mara kwa mara huambukizwa na hao hao wapenzi wao. Kwa kweli, asilimia 49% ya wanaougua huambukizwa na wapenzi wa kudumu. Hii ni kulingana na utafiti wa uswizi. Utumivu wa mpira wa kuaminika na kuutumia kwa njia sahihi unaeza kukuepusha kupata HIV wakati wa kujamiiana (katika uke au kupitia nyuma). Ngono ya sehemu ya nyuma pia inahitaji utumizi wa mpira, kwa kuwa uhusiano huu unauwezo mkubwa zaidi wa kuambukiza virus vya ukimwi kuliko uhusiano wa aina nyingine. Wengine husema uhusiano kutumia midomo (oral sex) ni hatari sana. Wataalamu wanasema hatari ya maambukizi kupitia uhusiano wa midomo ni ngumu kutathmini. "Katika utafiti uliofanywa kati ya miaka 1990 na 1992 kati ya wanume waliopatikana na HIV , sita kati ya wauguzi 37 (16.2%) walioambukizwa chini ya mwaka mmoja kabla ya kupimwa walitaja kuambukizwa kupitia uhusiano wa midomo."[1] Lakini kuna uwezo wa waliobaki kuambukizwa kupitia uhusiano wa midomo pia. Licha ya hayo,utafiti huu

unahusisha wanaume pekee. Maambukizo kupitia uhusiano wa midomo yanawezekana kwa wanawake pia. Aidha wanaume wanashauriwa kuepuka uhusiano wa kimapenzi na wanawake wakati wa hedhi.

Licha ya uhusiano wa ngono na anayeugua kutokana na virusi vya ukimwi, kuna njia nyingine za kuambukizwa na kujilinda. Kwa mfano, kuchangia sindano za kujidunga madawa ya kulevya. Mara kwa mara HIV hueenea katika watumizi wa madawa ya kulevya. Kuchangia sindano husababisha uwezekano mkubwa wa kuambukizwa katika jamii za watumizi wa madawa ya kulevya kwa sababu ya chembe ndogo za damu zilizoathirika ambazo sio rahisi kuona kwenye sindano. Hivyo basi, watumizi wa madawa watumie sindano za kibinafsi. Hata hivyo, ni nadra kwa wagonjwa kuambukizwa kwa ajali kupitia sindano zilizoathirika na wafanyakazi wa huduma za afya.

Kuambukizwa kwa kukutana na damu iliyoathirika bado ni shida kubwa katika nchi zinazoendelea. Nchi zilizoendelea zilirekebisha shida hii kwa kutumia njia za kufuatilia, kupima na kukanza damu (kukanza damu huua virusi vya HIV). Lakini kusini mwa Afrika hakuna fedha za kufanya hayo yote.

Njia nyingine ya kuenea kwa HIV ni kupitia mama mja mzito anayeugua kwenda kwa mtoto. Hii ni kupitia mtoto anapokuwa tumboni mwa mama, wakati wa kuzaliwa au kupitia maziwa yaliyoambukizwa ya mama. Hata hivyo, kuna njia za kupunguza uezekano wa kuenea kwa virusi. Kwanza kabisa kuna madawa ambayo yakitumika mama akiwa mja mzito hupunguza kwa wingi uwezekano wa kuenea wa ukimwi kati ya mama na mtoto. Aidha, mbinu ya kujifungua ya cesarean hupunguza uwezekano wa kuambukizwa. Mbinu hizi mbili pamoja hupunguza uwezekano wa mtoto kuambukizwa hadi asilimia 1.

Bila shaka, ni muhimu kuepuka matumizi ya maziwa ya mama anayeugua ili mtoto asiambukizwe hasaa baada ya kuzaliwa bila kuambukizwa. Mbinu hii hutekelezwa kwa urahisi katika nchi zilizoendelea. Katika nchi za kusini mwa Afrika, kwa sbabu ya gharama kubwa ya vyakula, wanawake wengi hawana budi ila kulisha watoto wao kwa maziwa ya mama.

Ijapokuwa haya yote hayapendezi, kuna habari njema. Hata ikiwa watu wameambukizwa na HIV, kuna uwezekano wa kusitisha kuenea kwa virusi mwilini na kuepuka mwanzo wa maradhi. Basi, PEP hutumika. PEP ni dawa ya kuongeza kinga ya mwili inayoweza kutumiwa muda mfupi baada ya kujihatarisha. Kujihatarisha, kwa mfano, ni kupitia wafanyakazi wa idara ya afya na katika uhusiano wa ngono

Matibabu haya ya baada ya kujihatarisha, PEP, yanaufanisi zaidi yanapotumiwa mapema. Kwa mfano, kuna uwezo mkubwa zaidi wa kuepukana na maambukizo PEP inapotumika kabla ya masaa mawili baada ya mahusiano ya kingono na anayeuguza kutokana na HIV. uwezekano wa kuepuka maradhi hupungua na wakati. PEP haina uwezo wa kumaliza kueenea kwa virusi vya HIV masaa ishirini na nne baada ya kujihatarisha.

PEP ni muhimu sana kwa idara ya afya. Wakati ambapo kinga ni chache na wauguzi ni wengi, bila shaka kuna uwezekano mkubwa wa wafanyakazi wa idara ya afya kuambukizwa. Upatikanaji wa PEP utapunguza uwezekano huu. PEP inafaa kuwa kati ya paketi ya tahadhari ya kimataifa inayopunguza kujihatarisha kwa wafanyakazi wa idara ya afya. Kwa hivo, inaaminika kuwa upatikanaji wa PEP kwa wafanyakazi wa idara ya afya unaeza kupunguza hofu za wafanyakazi kuhusiana na uwezo wa

kuambukizwa na ukimwi kazini. Hii inaeza kuwa motisha kwao kutoa huduma kwa walioambukizwa na ukimwi.

## Marejeo:

[1]http://www.phac-aspc.gc.ca/publicat/epiu-aepi/epi_update_may_04/13_e.html

http://www.sfaf.org/aids101/transmission.html

http://www.who.int/hiv/en/

http://www.who.int/hiv/topics/prophylaxis/en/

http://en.wikipedia.org/wiki/Aids

http://www.faz.net/s/RubDDBDABB9457A437BAA85A49C26FB23A0/Doc~E2FFCA35112524FEF9131137A6DE0922A~ATpl~Ecommon~Scontent.html

http://www.niaid.nih.gov/factsheets/hivinf.htm